

KILIO CHANGU

1. Ki - li - - o cha-ngu u-ki-ki-si-ki-a, u - fa nye ha-ra-ka ku-ni-sa - i - di-a,

na pi - ndi-shi - da zi-na-po-ni - ji - a, U - fa - nye ha-ra-ka ku-ni-sa - i - di a.

2. Ee Mungu wangu, ndiwe kimbilio,
Ewe Bwana wangu, ndiwe tegemeo.
Nikitaabika uje kwangu mbio,
Ewe ngome yangu, njoo kwangu, njoo.

3. Usinitupe wewe ndiwe kinga,
Mimi ni kondoo, wewe wanichunga.
Adui zangu zidi kuwapinga,
Na giza likija, nipayatia mwanga.

4. Daima wewe ni wangu msaada,
Bwana, usichoke zidi kunilinda.
Ukiwa nami sitapata shida,
Kwa uwezo wako, mimi nitashinda,

5. Uniepushe na mwovu shetani,
Ili asinitie majaribuni.
Mimi myonge nakutumaini.
Wewe uwe nami, nifike mbinguni.